


**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 4, Issue 1, 2019**
**ISSN: 1476-4687**

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# UTATA KATIKA UFUNDISHAJI WA ISIMUJAMII KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA

*Martha N. Wafula[1*], Dkt. Fred Simiyu Wanjala[2] & Dkt. Ben Nyongesa[3]*

[1]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, wafmartha@gmail.com.
[2]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, wsimiyu@kibu.ac.ke.
[3]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, bnyongesa@kibu.ac.ke.

**Article history:**

*Received: 19 Aug 2019*
*Accepted: 21 Aug 2019*
*Published: 23 Aug 2019*

**Keywords**:

*Utata,*
*Ufundishaji,*
*Isimujamii,*
*Kubaini,*
*Kiada,*
*Vipengele*

## IKISIRI

Makala haya yamelenga kubaini utata katika ufundishaji wa kipengele cha isimujamii katika shule za upili Kaunti ndogo ya Teso Kaskazini. Kipengele cha isimujamii kina umuhimu katika lugha ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano na mchango katika ufanisi wa mitihani. Ufundishaji wa isimujamii umekumbwa na malalamishi na lawama kutoka kwa walimu wa Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia lengo moja kuu ambalo ni kubaini chanzo cha utata katika ufundishaji wa isimujamii kwa kurejelea vitabu vya kiada. Malengo mengine ya mada ya utafiti yalikuwa pamoja na kupambanua mifumo ya uwasilishaji wa vipengele vya isimujamii katika vitabu vya kiada na kudadavua mikakati inayotumiwa kuvitathmini vipengele vya isimujamii katika shule za upili. Utafiti huu ulilenga kuvitazama vitabu vya kiada ili kubaini chanzo cha utata katika ufundishaji wa isimujamii. Mtafiti aliongozwa na nadharia ya uamilifu wa muktadha iliyoasisiwa na Thomas Stitch. Idadi ya walimu kumi na wanane wanaofundisha somo la Kiswahili kutoka shule teule walishirikishwa kwenye utafiti. Data asilia ilikusanywa kwa njia ya uchanganuzi wa matini na mahojiano ya ana kwa ana baina ya mtafiti na watafitiwa. Data ya utafiti ilichanganuliwa kwa mujibu wa malengo makuu ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia ya utafiti. Matokeo yaliwasilishwa kwa maelezo na asilimia. Matokeo yalionyesha kuwa vitabu vya kiada vinachangia utata uliopo katika ufundishaji wa isimujamii katika shule za upili. Hata hivyo utata uliopo unaweza kuondolewa iwapo utakabiliwa ipasavyo. Mtafiti alipendekeza kuwa vitabu vya kiada viangaliwe upya ili kuondoa udhaifu uliopo. Wizara ya elimu na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala (T. U. M. K) iweze kuidhinisha vitabu maalum vya kutumika kwa ufundishaji wa isimujamii katika shule za upili. Mtaala wowote kabla ya kuanzishwa ufanyiwe majaribio ili kutathmini ubora na udhaifu wa utendakazi wake.

## UTANGULIZI

Taaluma ya isimujamii imekua na kushamiri miaka ya 60 na 70 iliyopita. Kuna umuhimu kuelewa kimakini uhusiano kati ya lugha kwa taaluma iliyojiita isimu. Hata hivyo huu haukuwa mwanzo wa kulitazama suala la lugha kwa kuegemea misingi ya kijamii. Kwa miaka mingi lugha imekuwa ikitumiwa na wanajamii katika mahusiano yao.

Isimujamii hufunzwa katika shule mbalimbali za upili Afrika Mashariki kama mojawapo ya kipengele cha lugha. Vipengele vya isimujamii hufundishwa nchini Tanzania, Uganda, Kenya na Rwanda. Nchini Tanzania somo la isimujamii limeratibiwa kwenye mtaala na linafundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na kidato cha tao na sita kwa mujibu wa silabasi ya Tanzania mwaka (2005). Kwa mujibu wa Yohana (2005), mafunzo ya isimujamii yanaathirika kwa kiasi fulani kwa sababu ya ukosefu wa walimu na vitabu miongozo miongoni mwa mahitaji mengine ya elimu.

Mapendekezo ya Gachathi (1976) na Mackay (1985) yalichangia kutahiniwa kwa Kiswahili katika shule za upili na wanafunzi wa vyuo kufunzwa Kiswahili mwaka 1987. Tangu hapo kumekuwa na marekebisho kadha katika silabasi lakini mapitio ya mwaka wa 2002 yakawa ya umuhimu zaidi. Taasisi iliipa shughuli hii mapitio ya usawazaji wa silabasi ambayo iliupa mtaala sifa mpya kama vile kujumuisha isimujamii katika lugha ya Kiswahili na kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa.

Nchini Kenya, mafunzo ya isimujamii hujitokeza katika sehemu mbalimbali za lugha ya Kiswahili chini ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Lengo kuu katika silabasi ni kujenga haiba ya mwanafunzi, uwezo wake wa kuwasiliana, kurutubisha uwezo wa kuhusiana na watu wengine na kujiendeleza kielimu. Kulingana na Bishop (1985), ubora wa silabasi si uzuri wa yaliyomo tu bali ni utekelezaji wake. Zipo lawama kutoka kwa walimu kuwa pana changamoto katika kuvitekeleza vipengele vya isimujamii vilivyoingizwa kwenye silabasi ya Kiswahili miaka michache ya nyuma. Msukumo wa utafiti huu umetokana na sababu kuwa utekelezaji wa mafunzo ya isimujamii unakumbwa na changamoto zinazozua utata katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Utafiti wa Yohana (2005) kuhusu hali ya Kiswahili katika shule za upili Tanzania uliangaziwa mno. Semina ziliandaliwa ili kujadiliana na ubadilishaji wa taaluma katika ufundishaji wa Kiswahili baina ya walimu wa shule za upili wanaofunza Kiswahili na wataalam wa Kiswahili kutoka TUKI, TATAKI, na idara zote za Kiswahili za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Malengo yalikuwa kutathmini hali ya somo la Kiswahili na masomo yake kama isimujamii, fasihi, lugha na sarufi pamoja na kuainisha matatizo yanayowapata walimu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Utafiti huu ulibaini kuwa hapana utoshelevu wa muhtasari wa Kiswahili (1996). Hakukuwepo mada maalum zilizopangwa ili kutofautisha bayana viwango vya vidato.

Kihore (2005) anasema kuwa uchambuzi uliofanywa na walimu waliohudhuria semina huko Arusha mnamo Agosti tarehe 10 mwaka wa 2014 kuhusu mafunzo ya isimujamii na masomo mengine ya lugha ulionyesha kuwa muhtasari wa masomo haya una kasoro nne kuu ambazo zimechangia matatizo katika ufundishaji wa kipengele cha isimujamii. Kwanza, ukosefu wa mpangilio maalum wa mada za ufundishaji; pili, vipengele vidogo vinajirudiwarudiwa bila kuonyesha tofauti ya uchanganuzi wa kina wa mada kwa kila kidato; tatu, mada hazina vitabu maalum vya kiada vinavyoelezea nadharia; na nne, kuweko kwa vitabu vinavyozidisha na kupunguza maandishi ya kitaaluma ni changamoto nyingine inayokabiliwa. Hali hizi ni moja wapo ya matatizo na changamoto kuu katika ufundishaji wa isimujamii na masomo mengine ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

Niyomugabo (2005) anasema kuwa nchini Rwanda, kuna matatizo ya ufundishaji na usomaji wa lugha yakiwemo matatizo ya kimaongezi, kimaandishi, ukosefu wa walimu, vifaa vya kufundishia, uhaba wa vitabu makala pamoja na matatizo ya sera ya elimu. Anaendelea kusema kuwa matatizo ya kukosa vitabu, vifaa vya kiteknolojia kama redio, televisheni pamoja na

uhaba wa walimu yanatatiza ufundishaji. Walimu wanafundisha masomo ya isimu kama lugha ya kigeni kwa sababu wengi hawajachukua mafunzo ya kazi ya ufundishaji. Odeo (2007) katika utafiti wake anasema kuwa silabasi mpya iliyoanzishwa inatatiza kiutekelezaji kwani baadhi ya mafunzo ya sarufi yalilenga kiwango cha chuo kikuu. Anaendelea kusema kuwa ugumu wa mada unawatisha wanafunzi na kuwafanya wachukie somo la Kiswahili. Baadhi ya istilahi zilizotumika haziafiki kiwango cha wanafunzi wa shule za upili hivyo inakuwa vigumu wao kuelewa baadhi ya istilahi zilizotumika katika mafunzo ya sarufi.

Mwangi (2008) anasema kuwa walimu wanaonyesha hofu kuhusu udhaifu wa mtaala wa isimujamii. Utafiti huu umeonyesha maoni ya walimu na wataalam wa mitaala kuhusu hatua zinazoweza kufuatwa katika uundaji na utayarishaji wa mtaala ili kuepuka athari ya utendakazi wa mtaala huu. Anapendekeza kuwa mafunzo na mikakati katika ufundishaji wa isimujamii yachunguzwe kwa undani ili kubaini matatizo yanayokabili ufundishaji wa kipengele cha isimujamii kwa shule za upili nchini Kenya.

Okwany (1993) naye alitafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya kuhusu ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kazi hiyo ilionyesha kuwa mielekeo ni zao la jamii na husababishwa na utamaduni wa jamii ambamo lugha mbalimbali huzungumzwa. Utafiti wake uliweza kubainisha kuwa wanafunzi wengi wana mwelekeo chanya wa kijumla kuhusu lugha ya Kiswahili. Jambo hili kwa mujibu wa Okwany (1993) labda limechangiwa na Kiswahili kufanywa somo rasmi shuleni na linalotahiniwa kwenye mitihani ya kitaifa katika shule za msingi na upili nchini Kenya. Mapendekezo yaliyotolewa kuboresha ujifunzaji wa Kiswahili yalichangia kuelezea na kufafanua mapendekezo ya utafiti huu. Aidha maoni yaliyodhihirishwa kuhusu mielekeo chanya ya wanafunzi yalichangia katika kutoa mapendekezo zaidi kwa asasi mbalimbali za elimu ili kuinawiri taaluma ya isimujami. Kwa mujibu huu, lengo kuu la utafiti huu ulikuwa kubaini chanzo cha utata katika ufundishaji wa isimujamii kwa kurejelea vitabu vya kiada.

## MBINU ZA KITAFITI

Kothari (2008) anaeleza kwamba, utafiti wowote uwe wa kitaaluma ni lazima ufanywe kwa kuongozwa na mbinu mbalimbali za utafiti ili uweze kutoa matokeo yasiyo na shaka ndani yake. Utafiti huu ulitumia muundo wa usoroveya elezi mkabala wa kithamano. Utafiti huu ulilenga kubaini chanzo cha utata katika ufundishaji wa vipengele vya isimujamii kwa kurejelea vitabu vya kiada. Katika lengo hili mtafiti alichunguza iwapo vipengele vyote vilivyoorodheshwa kwenye vitabu vya kiada vipo kwenye silabasi, mpangilio wa vipengele iwapo vinatiririka na pia iwapo vimebainishwa au la.

Vitabu vya kiada vilivyotumiwa viliteuliwa kimakusudi. Hivi vilikuwa pamoja na Kiswahili Kitukuzwe, Chemchemi za Kiswahili na Kiswahili Fasaha kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Vitabu hivi viliteuliwa kwa kutumia sampuli kusudio maana ndivyo tu vilivyoratibiwa rasmi na Wizara ya elimu pamoja na Taasisi Kuu ya Ukuzaji wa Mitaala (T. K.U. M) kutumika kufunzia lugha ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Vitabu vya kiada na silabasi ya isimujamii vilitumika kama sampuli muhimu zaidi katika utafiti huu.

Mtafiti vilevile alichunguza maandalizi ya walimu katika maazimio ya kazi na andalio la somo ili kumsaidia kueleza kikamilifu utata uliopo katika ufundishaji wa kipengele cha isimujamii.

Njia ya uchambuzi wa matini ilimwezesha mtafiti kutazama makosa yaliyopo kwenye vitabu vya kiada kwa kulinganisha na silabasi. Utazamaji huu pia ulimwezesha kubaini iwapo vipengele vimepangwa kwa njia ya kutiririka na iwapo vimebainishwa au la.

Data nyingine ilikusanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa. Walimu walihojiwa kuhusu mifumo tofauti ya kuviratibu vipengele vya isimujamii kwenye maazimio ya kazi.

Asilimia 30 ya shule zote 31 zilihusishwa kwenye utafiti. Mugenda na Mugenda (2003) anasema kuwa kikundi kidogo kiwe asilimia 30 ya kundi zima. Matokeo yakawa idadi ya shule 9 zilizokuwa za kategoria za kitaifa, kaunti, kaunti ndogo, za

kibinafsi, mseto, kutwa, wavulana pekee na wasichana. Mtafiti aliteua walimu wawili wanaofundisha Kiswahili kutoka shule tisa (9) zilizoteuliwa hivyo kupata jumla ya watafitiwa kumi na wanane (18). Kati ya shule hizi tisa, nne (4) zilikuwa na walimu wawili tu wa Kiswahili ambao waliteuliwa kutumia sampuli kusudi maana wawili walihitajika kutoka kila shule. Shule tano zilizosalia zilikuwa na walimu zaidi ya watatu.

Mtafiti alitaka kujiepusha na ubaguzi akaweza kuorodhesha majina ya wasailiwa kwenye vijikaratasi na chini ya majina akaandika 'nitashiriki' vingine 'sitashiriki' kwa hivyo wasailiwa wawili kutoka kila shule walioteua nitashiriki ndio walishirikishwa kwenye utafiti. Babbie (2014) anasema kuwa tafiti nyingi zinazohusu sayansi ya jamii hazitumii sampuli nasibu kwa wingi katika uteuzi wa sampuli zao bali huegemea katika mbinu zisizo za kinasibu kuteua sampuli kama vile sampuli kusudio.

Utazamaji wa vitabu, maazimio ya kazi na andalio la somo ulimwezesha mtafiti kupata data aliyotarajia kasha ikachanganuliwa kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya utafiti.

## MATOKEO YA UTAFITI

Katika hatua ya kwanza ya kuchunguza vipengele vyote vilivyopo kwenye silabasi vipo kwenye vitabu vya kiada, mtafiti aligundua kuwa asilimia (95) ya vipengele vya isimujamii vilivyoorodheshwa kwenye silabasi vimeweza kushughulikiwa katika vitabu vya kiada. Uchunguzi wa kina wa vitabu vya kiada ulifichua kuwa baadhi ya vitabu vya kiada vimeorodhesha idadi chache ya vipengele ikilinganishwa na idadi iliyoko kwenye silabasi. Tukiwarejelea Wamitila na Wahiga kidato cha tatu vipengele vyote vilivyopo kwenye silabasi vinavyofaa kufundishwa kidato cha tatu vimeweza kuorodheshwa isipokuwa mazungumzo katika mazingira ya kuabudu.

Uchunguzi ulionyesha kuwa vipengele vingine vilivyopo kwenye vitabu vya kiada havijaorodheshwa kwenye silabasi. Tukiwarejelea Wahiga na Wamitila kidato cha kwanza, kipengele cha kwanza kilichoshughulikiwa hakipo kwenye silabasi kabisa. Huenda waandishi wanajiongezea vipengele vya isimujamii ambavyo wanaona vitasaidia kujifunza isimujamii ambavyo havijaorodheshwa na kufundishwa popote kwenye silabasi.

Iligundulika kuwa baadhi ya vipengele vya isimujamii kwenye vitabu vya kiada havijabainishwa. Rejelea Makombo na wenzake kidato cha kwanza sura ya 4, 6 na 7, kidato cha pili sura ya 20, kidato cha 4 sura ya 4, 6, 7 na 8. Tukiwarejelea Waititu na wenzake kidato cha kwanza hapana popote palipoelekezwa kuwa isimujamii japo vipengele vya isimujamii vimejitokeza katika stadi ya kusikikiza na kuzungumza.

Matokeo yalionyesha pia kuwa vipengele vya isimujamii havitiririki, vimetapakaa kwenye sura mbalimbali bila kubainishwa kwa hivyo mwalimu anahitaji muda wa kuvitenga ili kuvishughulikia moja kwa moja kama isimujamii. Jambo hili linawaathiri walimu hivyo wanashughulikia isimujamii kwa njia tofauti.

Utazamaji wa maazimio ya kazi ulimwezesha mtafiti kubaini kuwa kuna utofauti katika kuviratibu vipengele vya isimujamii kwa sababu ya mifumo tofauti ya uwasilishaji iliyoko kwenye vitabu vya kiada. Hali hii pia imechangia utofauti wa kuainisha shabaha hivyo kuathiri uteuzi wa vifaa vya kufundishia.

Mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa yalionyesha pia kuwa vifaa vinatumika kwa uchache na vichache vinavyotumika vingine havisaidii kuelewa dhana za isimujamii ipasavyo. Hivyo vipengele vingi vya isimujamii katika shule za upili vinafunzwa na kueleweka kwa njia ya kidhahania.

Asilimia 80 ambao ni walimu 15 walimtajia mtafiti tatizo la vitabu vya kiada kubainisha baadhi ya vipengele vya isimujamii limekuwa likiwapa changamoto katika ufundishaji. Huenda pia wanaathirika na mifumo tofauti iliyotumika kwenye vitabu vya kiada kuviwasilisha vipengele vya isimujamii. Maazimio ya kazi yalionyesha kuwa walimu wengi wanafundisha somo hili kutokana na tajriba waliyonayo. Inabainika kuwa pana udhaifu katika mtaala wa isimujamii. Kipengele cha isimujamii kina utata kiutekelezaji.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.**

Makala haya yameangazia utata katika ufundishaji wa isimujamii kwa kuchunguza iwapo vioengele vyote vilivyoorodheshwa kwenye silabasi vipo. Uchunguzi ulifichua kuwa vipengele vingi vilivyoorodheshwa kwenye silabasi vipo kwenye vitabu vya kiada japo kuna baadhi yavyo vipo kwenye vitabu vya kiada lakini havipo kwenye silabasi. Vilevile vipo baadhi ya vipengele vinavyolenga isimujamii japo havijabainishwa kwenye vitabu vya kiada. Vipengele vingi vya isimujamii havitiririki kwani vimetapakaa na vinajitokeza kwenye sura mbalimbali za vipengele vya lugha bila kubainishwa. Mwalimu anahitaji kutenga muda na kuwaelekeza wanafunzi kuwa vinalenga isimujamii. Hali hii imechangia utata uliopo katika ufundishaji wa isimujamii.

Aidha utazamaji wa maazimio ya kazi unadhihirisha namna tofauti jinsi walimu wanavyofundisha vipengele vha isimujamii. Maandalizi ya vifaa vya ufundishaji pia ni changamoto maana hapana utaratibu maalum wa kutekeleza isimujamii. Hivyo walimu wanaathirika na utaratibu uliopo kwenye vitabu vya kiada ambao unazua utata katika ufundishaji wa isimujamii.

Kutokana na matokeo haya, inapendekezwa kuwa vitabu vya kiada vichunguzwe upya ili kuondoa udhaifu uliopo kwa nia ya kuboresha mafunzo ya isimujamii. Shughuli hii ihusishe washikadau wote ikiwemo walimu wa somo la Kiswahili. Inapendekezwa kuwa vitabu maalum vya isimujamii viandikwe na kuidhinishwa na Wizara ya elimu kwa ushirikiano na (T.K.U.M) ili kuboresha mafunzo ya isimujamii. Kabla ya mtaala wowote wa lugha kuanzishwa, majaribio ya kutosha yafanywe ili kutathmini ubora na udhaifu wa utendakazi wa mtaala huo. Tathmini hii itasaidia kuondoa changamoto zinazoweza kutokea kwenye mtaala huo.

MAREJELEO


Best, W. J. na Kahn, J.V. (2010). *Research in Education*. New Jersey, U. S. A: Person.

Bishop, G. (1985). *Curriculum Development: A Textbook for Students*. London: Macmillan Education Ltd.

Kenya Institute of Curriculum Development (2002). *Secondary school Syllabus* (Vol.1.). Nairobi: Government printers.

Kenya National Examination Council (2005). *Kenya Certificate of Secondary Education 2004 Candidates Performance Report*. Nairobi: Kenya.

Kihore, M. (2005). Ufundishaji wa Sarufi Miundo ya Kiswahili katika Shule za Sekondari Tanzania. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili 2000* (uk 109-121.), imehaririwa na J.S. Mdee na H.J.M. Mwansoko. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa kiswahili na chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Kothari, C.R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.

Makombo na wenzake. (1987). *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 1-4*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ministry of Education Science and Technology (2002). *Secondary Education Syllabus* (Volume One). Nairobi: Kenya Institute of Education.

Mugenda, A. na Mugenda, O. (2003). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Kenya Act Press.

Mwangi, B. (2008). *Mikakati iliyobuniwa kwa ufundishaji wa isimujamii katika shule za upili*. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Kakamega na Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Niyomugabo, C. (2012). Kinyafrangles of a newly created language in Rwanda. *Rwandan journal of Education*, 1(1) 19-28.

Odeo, I. (2007). Utekelezaji wa Silabasi Mpya ya somo la Kiswahili katika Shule za upili: Mtazamo

wa walimu. Katika Mkopi, K. (Mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya.* Limuni: Kolbe Press.

Okwany, L. (1993). *Attitude of High School Students in Kenya towards Learning of Kiswahili.* Canada: University of New Brunswick.

Wahiga, G. na Wamitila, K. (2003). *Chemchemi za Kiswahili kidato cha pili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Waititu, F. na Ipara, O. (2005*). Kiswahili Fasaha Kidato cha 1-4.* Nairobi: Oxford University press.

Yohana, B. A. (1919). *The Yao: Chikala cha Wayao*. London: Rrank Cass and Compony Limited.